**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI KOROGWE**

**SHULE YA SEKONDARI NGOMBEZI**

S.L.P 63, Korogwe-Tanga, Barua pepe:ngombeziss@korogwetc.go.tz, Simu/Contc
Mkuu wa Shule-0784848040, Makamu Mkuu wa Shule-0714786812, 0756346200

**Kumb.Na. NGSS/AL/20/05/2026/2027** **Tarehe…………………….**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………………………………………….…….
S.L.P…………………………………………………….
………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGOMBEZI MWAKA………………….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato cha tano** Tahasusi ya …………. katika shule hii mwaka…………………. Shule ya sekondari Ngombezi ipo umbali wa Kilometa tatu kutoka kituo cha mabasi cha mji wa Korogwe. Usafiri wa Bajaji/pikipiki unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mji wa Korogwe. Nauli ni shilingi elfu mbili mpaka elfu tatu.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe………………. Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe…………………. na mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………………..

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**(A) SARE YA SHULE HII NI: -**

i. Suruali mbili kitambaa kizito cha suti rangi ya Kijani Jeshi yenye marinda mawili ya nusu
ii. nchi na turn-up chini (isiwe modal/kubana) kwa wavulana.
iii. Suruali 2 za blue iliyokolea kwa matumizi ya nje ya darasa (***isiwe modal***) kwa wavulana.
iv. Sweta rangi ya Kijani Jeshi shingo ya V, unaweza kuzipata duka la shule kwa bei ya shilingi 15,000/= ukipenda.
v. T-Shirt 3 (tatu), mbili (2) za rangi ya dark blue za kushindia na moja (1) ya rangi ya brown ni ya kuvaa darasani, unaweza kuzipata shuleni ukipenda kwa bei ya shilingi 15,000/= (kumi na tano elfu tu kwa moja).
vi. Mashati mawili meupe (Tetron) mikono mifupi.
vii. Sare ya viatu vya darasani ni viatu vyeusi vya kufunga kamba (Jozi mbili) visiwe na kisigino.
viii. Soksi jozi mbili au zaidi nyeupe.

**(B) SARE YA MICHEZO KWA SHULE HII NI KAMA IFUATAVYO: -**

(i). Bukta rangi bluu inayofika kwenye magoti.
(ii). Track suti rangi ya blue iliyokolea (dark blue)
(iii). Viatu vya michezo. (Njumu)

**(C) MAHITAJI MENGINE ANAYOPASWA MWANAFUNZI KUJA NAYO SHULENI: -**

i. Ndoo mbili (lita 10) zenye mfuniko, sahani/bakuli, kijiko na kikombe.
ii. Shuka mbili au zaidi za rangi ya blue bahari kwa wavulana.
iii. Taulo la kuogea, malapa, mswaki, Mto, Foronya ya mto ifanane na rangi ya shuka
iv. Dawa ya kusafishia vyooni ARO moja na Sabuni ya vyooni Galoni moja (HKL na KLF)
v. Godoro **JIPYA** lenye unene usiopungua inchi 3, upana futi 2.5 na urefu futi 6.
vi. Sanduku la bati pamoja na Chandarua kimoja cha pembe nne.
vii. Madaftali makubwa (Q3) yasiyopungua 14, kalamu za kutosha na Kamusi/ Dictionary.
viii. Vitabu vya dini na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi.
ix. Ream ya Karatasi (A4) plain (1) kwa mwaka. (Kampuni ya A ONE au nyingine **isiwe kampuni ya MONDI** na Ream moja yenye mistari kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi.
x. Jembe Jipya lenye mpini (HKL na KLF), Panga moja (HKL) na Fagio moja soft au Hard broom kwa ajili ya usafi (KLF).
xi. **Kadi ya Bima ya Afya. Kama hana bima ya afya awe na fedha binafsi ya dharura.**

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI: -**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 60,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 10,000.00 |
| 3 | Kitambulisho | 5,000.00 |
| 4 | Nembo | 5,000.00 |
| | **JUMLA** | **80,000.00** |

**N.B.**

*Fedha hiyo Tshs **80,000.00** ilipwe kwenye Akaunti ya shule **41501200088** NMB Jina **Ngombezi Sec School** kwa Wakala wa NMB au tawi lolote na mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki ikiwa imeandikwa jina sahihi la mwanafunzi.*

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi kama ifuatavyo: -

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo nchi na zisiwe zimewekwa dawa.
j) Shuleni hakuna kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na pambo la aina yoyote. (Mkufu,hereni, pete, Marashi n.k)**

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kutoa lugha Chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
4. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
5. Uasherati/Uzinzi, Mahusiano ya kimapenzi jinsi moja au jinsi tofauti.
6. Ubakaji/ Ulawiti na Ushoga
7. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, Sigara, cocain, mirungi,kubeli n. k.
8. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
10. Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kudharau bendera ya Taifa
12. Kuoa au kuolewa
13. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote cha umeme.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
18. Kukaa bwenini au kulala wakati wa vipindi au kazi za nje za shule, Kunyanyapaaa wengine.
19. Kususia/kukataa kufanya mitihani ya ndani na nje ya shule kwa makusudi.

**4.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Nakala ya matokeo ya Kidato cha IV (Result slip) na ya cheti cha Kuzaliwa mwanafunzi.
b) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti
c) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
d) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatolewayo na shule.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana Ngombezi Sekondari.

BENO V. MSOFE
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
NGOMBEZI SEKONDARI
S.L.P 63, KOROGWE

**SHULE YA SEKONDARI NGOMBEZI**
**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi (Majina kamili) …………………………………………………………………….…...
Nimekubali kuingia kidato cha …………… katika Shule ya Sekondari Ngombezi Korogwe kuanzia tarehe ………………….. hadi nitakapomaliza kidato cha …………
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa …………….…………………… Kijiji/Mtaa …………….………. Tarafa ……………………………………. Wilaya ……………………………... Shule unakotoka ……………………………………………………………………………………….
Namba yako ya mtihani……………………………………………………………………….
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako………..………….
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ……………………… Saini ya mwanafunzi ……………………. Tarehe ………………………...

**B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI**

1. Mimi (Jina kamili) …………………………………… simu…………………… ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari Ngombezi kuanzia kidato cha …………hadi atakapomaliza kidato cha ..……………
2. Jina kamili la Mama………………………………………… Kazi ya Mama……………………… Simu……………………………….
3. Kazi ya Baba …………………………………….. Simu……………………………….
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………….
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura
Jina kamili Mahusiano Anakoishi Simu yake
(i)……………………………… …..…………… ………………. …………………
(ii) ……………………………… …..…………… ………………. …………………
(iii) ……………………………… …..…………… ………………. …………………
(iv) ……………………………… …..…………… ………………. …………………
6. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa……………………………….
Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………… Tarehe …………………………

BENO V. MSOFE
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
NGOMBEZI SEKONDARI
S.L.P 63, KOROGWE

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION**
**KOROGWE TOWN COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**NGOMBEZI SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 63,**
**KOROGWE.**
**DATE………………………**

**MEDICAL OFFICER………………………...……...**

**GOVERNMENT HOSPITAL, ………………………………………………………………**

**NAME OF STUDENT……………………………………………………………………...**

Please examine the above-named Student to ascertain her fitness for further studies.

THE HEAD MASTER
NGOMBEZI SEC. SCHOOL
P.O.BOX 63, KOROGWE

**THE HEAD MASTER**
**NGOMBEZI SEC. SCHOOL**

**MEDICAL CERTIFICATE** I have examined the above named with regard to:

Skin…………………………………………………………………………………………
Eyes…………………………………………………………………………………………
Ears…………………………………………………………………………………………
Chest………………………………………………………………………………………..
Spleen………………………………………………………………………………………
Abdomen……………………………………………………………………………………
Urine………………………………………………………………………………………...
Stool…………………………………………………………………………………………
Hemoglobin…………………………………………………………………………………

**And I considered:**

1. He is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. He is now fit to return to school having treatment for…………………………………………. ……………………………………………………………………………………………….

**And I considered:**

3. He is now fit to return to school having checked for……………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..

| | | |
|---|---|---|
| ……… …………………… | ……………………… | …………… |
| NAME OF MEDICAL OFFICER | SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER | DATE |